Maswali Yanayoulizwa Mara Kwa Kara Kuhusu Virusi ya Corona

Mlipuko wa ugonjwa wa kupumua unaosababishwa na coronavirus mpya, inayojulikana kama COVID-19, inasababisha wasiwasi lakini sio hofu. UVM Health Network unashirikiana na Vermont State Health Department na New York State Department of Health kuratibu juhudi zetu za kujitayarisha kulingana na mwongozo kutoka kwa Centers for Disease Control and Prevention (CDC). Kipaumbele chetu cha juu bado ni kupeana huduma salama, bora kwa wagonjwa wetu wote.

Hapo chini utapata habari zaidi juu ya jinsi ya kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa coronavirus na hatua za kuchukua ikiwa wewe au mpendwa wako ameonyesha dalili za ugonjwa.

KUMBUKA! Ikiwa una homa, kikohozi na/au upungufu wa pumzi, ikiwezekana, pigia simu ofisi yako ya kwanza ya utunzaji kuzungumza na mtoaji wa utunzaji.

Huduma ya nyumbani inaweza kuwa chaguo bora kwa watu wengi wa jamii yetu ambao wanaugua.

VIRUSI YA CORONA NI NINI?

Kulingana na World Health Organization (WHO): Coronaviruses ni familia kubwa ya virusi ambayo inaweza kusababisha magonjwa ya kupumua kwa wanadamu, kutoka kwa homa ya kawaida hadi magonjwa mazito kama vile Middle East Respiratory Syndrome (MERS) na Severe Acute Respiratory Syndrome (SARS) . COVID-19 ni ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na coronavirus iliyogunduliwa hivi karibuni. Virusi na ugonjwa hii mpya haukujulikana kabla ya kuzuka kuanzia huko Wuhan, Uchina, mnamo Desemba 2019.

DALILI ZAKE NI NINI AND ZINAFANANAJE NA ZILE ZA HOMA AMA HOMA YA KAWAIDA?

Dalili ni kikohozi, homa na upungufu wa pumzi. Dalili ni sawa na zile za homa, ingawa hii inaaminika kuwa kubwa zaidi kuliko homa.

Ikiwa una homa, kikohozi na/au upungufu wa pumzi, ikiwezekana, pigia simu ofisi yako ya kwanza ya utunzaji kuzungumza na mtoaji wa utunzaji.

INAZAMBAZWA VIPI?

COVID-19 inaenea kupitia matone hewani, kwa hivyo kukohoa na kupiga chafya kunaweza kuenea kwa watu wa karibu. Inawezekana kwamba inaweza kuchafua/kuenea kwa vitu vingine pia. Muda ya kuonyesha dalili hufikiriwa kuwa siku 14, hata hivyo hii inaweza kubadilika kadiri virusi vinavyoeleweka.

NAWEZAJE KUZUIA?

Njia za kimsingi za kuzuia ni zile ambazo tunapaswa kuzitumia wakati wote:

Osha mikono yako mara kwa mara - tumia dawa ya ku osha mkono, na osha mikono yako kabla ya kula. Usiguse uso wako. Usiende penye kuna watu wengi. Usisafiri kwenda nchi ambazo CDC imeangazia kuwa ina maambukizi mengi. Kukaa mbali na penye watu wengi itazidi kuwa muhimu zaidi - shule zetu, mikutano na shughuli zingine zilizopangwa zitahitajika kuzingatia jambo hili kesi kwa kesi.

Ikiwa wewe ni mgonjwa, kaa nyumbani. Safisha mikono yako. Osha vitu venye matumizi ya juu kila siku. Ikiwa uko mahali ambapo virusi vinazunguka zaidi, pigia daktari wako wa huduma ya msingi kupata ushauri. Usiende kwa Huduma ya Dharura au Idara ya Dharura isipokuwa unayo upungufu wa pumzi, au vinginevyo unahitaji msaada wa matibabu wa haraka.

Tafuta nini unaweza kufanya ili kuepushaana na Coronavirus-19. VIDEO

HIVI MAJUZI NIMERUDI KUTOKE KUSAFIRI NA SASA NINA KIKOHOZI. JE! NIPASWA KUINGIA ILI KUPIMWA?

Jambo la kwanza unapaswa kufanya ni kupigia simu kwa ofisi ya daktari wako na ueleze dalili zako. Kuna homa nyingi inayo zunguka, na dalili ni zinafanana. Hatutaki uende kwa Idara ya Dharura au Huduma ya Dharura kwa haraka bila lazima.

NINA KIKOHOZI NA HOMA. NIFANYE NINI?

Ikiwa wewe ni mgonjwa, kaa nyumbani, fanya mazoezi ya afya ya ku osha mikono, na ufunike kinywa chako na pua wakati wa kukohoa na kupiga chafya.

Pigia simu daktari wako na ueleze dalili zako. Wataweza kukushauri juu ya hatua za kufuata.

INAAMULIWAJE WAKATI MTU ANAHITAJI KUPIMWA?

Hivi sasa, kuna vigezo fulani na Vermont State Department of Health, New York State Department of Health na CDC ili kufanya uchunguzi. Lakini, kadiri wakati unavyoendelea, hii inaweza kuwa uchunguzi wa kawaida mara kwa mara.

INA MATIBABU?

Hivi sasa hakuna matibabu inayojulikana ya kuthibitika. Kuna dawa za majaribio zinasomewa. Lakini, katika hali kali zaidi, wagonjwa wanaweza kupata huduma ya msaada (oksijeni, maji ya IV, nk), ikiwa inahitajika.

JE! TUMEJIANDAA?

Kipaumbele cha juu cha UVM Health Network ni kutoa huduma bora kwa wagonjwa ilhali wanapeana nafasi salama kwa wafanyikazi. Itifaki za majibu zilitengenezwa kupitia uzoefu muhimu wa shirika na hali kama hizo za utunzaji wa afya. Timu ya watu tofauti inaratibu kuratibu utayari na mipango kama habari zaidi inavyoingia kutoka kote duniani. Kikundi hicho kinajumuisha watoa huduma ya afya ya mstari wa mbele, uongozi wa juu, kituo cha wagonjwa, usimamizi wa usambazaji, usafi wa viwanda, waalimu wa wafanyikazi, wataalam wa utayari wa hali ya dharura, usimamizi wa vifaa, maduka ya dawa, mawasiliano, kuzuia maambukizi na magonjwa ya kuambukiza. UVM Health Network unaendelea kupata habari na mapendekezo kutoka CDC, Vermont Department of Health na New York State Department of Health.

NIWE NA WASIWASI AINA GANI?

Ilhali dalili zinatafuatia kuanzia kidogo hadi kali (kwa wale watu walio na shida za kiafya), watu wengi wana ugonjwa wa kupumua kwa usawa. Ni muhimu kukumbuka kuna virusi vingine kadhaa vya kupumua vilivyo katika mkoa wetu ikiwa pamoja yao na mafua. Hajachelewa sana kupata chanjo chako cha mafua!